**Vyuo vya VETA Namtumbo na Songea vitakavyochochea uchumi wa viwanda mkoani Ruvuma**

**VETA Songea kuanzisha kozi za utalii na zana za kilimo**

**Na Albano Midelo**

MRADI wa chuo cha ufundi stadi VETA cha Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma unatekelezwa na serikali ya Tanzania kwa kutumia fedha za ndani kwa asilimia 100.



Mkandarasi Mkuu wa mradi huu ni Kampuni ya CF Builders Limited ambaye anatekeleza mradi huo kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 6.32.

Mhandisi Peter Siizya wa VETA Makao makuu akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo kwa Naibu Waziri wa Elimu,Sayansi na Teknolojia William Ole Nasha,anazitaja gharama hizo kuwa ni pamoja na kodi ya ongezeko la thamani(VAT).

Kwa mujibu wa Mhandisi Siizya katika kiasi hicho,Mkandarasi amelipwa zaidi ya shilingi bilioni 3.359 na kwamba Mshauri Elekezi

wa Mradi huo ni Kampuni ya Archquants Services Ltd yenye makao makuu yake jijini Dar es salaam ambayo inatekeleza mradi huo kwa mkataba wenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 171.

Hata hivyo Mhandisi Siizya anasema hadi sasa Mshauri Eelekezi amelipwa zaidi ya shilingi milioni 147 na kwamba mradi huo ni wa miezi 18 ambao mkataba wake umeanza Machi 18,2018 na ulitarajiwa kukamilika na kukabidhiwa Septemba 17,2018.

“Moja ya sababu ambazo zimechangia kuchelewesha mradi kukamilika kwa wakati ni Mkandarasi amechelesha, michoro ya kazi za nje ya chuo,akikamilisha michoro kazi itakamilika kwa asilimia 100”,anasisitiza Siizya.




“Mradi huu unajumuisha ujenzi wa majengo 14 pamoja na kazi ya kutengeneza mazingira ya nje.Majengo yanayojengwa ni jengo la

utawala,madarasa manne,vyoo,jengo la karakana ya ufundi bomba na ushonaji",amesema.

Anayataja majengo mengine kuwa ni karakana ya useremala,uashi,umakenika wa mitambo mizito,karakana ya umeme wa majumbani,jengo la maktaba,jengo la stoo na kibanda cha jenereta.

Anasema chuo hicho kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kutoa mafunzo ya ufundi stadi kwa wanafunzi 360 katika fani sita ambazo ni ushonaji wa nguo,ufundi bomba, useremala, uashi, umakanika wa mitambo mikubwa na ufundi umeme wa majumbani.

Kwa upande wake Mkuu wa Chuo cha VETA Songea Gideon Ole Lairumbe akitoa taarifa fupi ya chuo hicho kwa Waziri Nasha amesema chuo hicho kilifunguliwa rasmi Julai 20,2003 na Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda.

Lairumbe anayataja mafanikio ambayo chuo hicho kimeyapata kuwa ni pamoja na uwezo wa kudahili wanachuo umeongezeka toka wanafunzi 60 hadi 250 kwa mwaka katika kozi ya muda mrefu.




Anazitaja kozi hizo kuwa ni ufundi magari, ushonaji,umeme wa

majumbani,umeme wa magari, uashi,useremala,uhazili na kompyuta,ufundi mabomba na kuunga vyuma.

Hata hivyo Mkuu huyu wa chuo anasema,kutokana na wimbi kubwa la vijana kuhitaji kusoma mafunzo ya ufundi,chuo kimeanzisha masomo kwa awamu ya asubuhi na mchana ambapo mwaka huu chuo kimeanza na wanachuo 559.

“Kwa kutambua umuhimu wa ufundi stadi kwa maendeleo ya viwanda,chuo cha VETA Songea kinatoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi,wanachuo wanaoendelea na masomo wapo 560 kati yao wanaume 410 na wanawake 150”,anasema Laurumbe.

Katika hatua nyingine ya maendeleo ,Mkuu huyo wa chuo cha VETA Songea,anasema chuo kimeanzisha mafunzo ya masafa ambapo hivi sasa kuna mafunzo ya muda mfupi katika Mkoa wa Njombe,Mbinga,Ludewa,Ikonda,Tunduru na Namtumbo.

Anabainisha zaidi kuwa chuo hicho kinatoa mafunzo kwa kushirikiana na viwanda kwa lengo la kuwajengea uweo zaidi wafanyakazi viwandani ili kuongeza tija.

Anasema hadi sasa chuo kimeshirikiana  na viwanda mbalimbali vikiwemo viwanda vya  chai cha Uniliver Njombe,Kampuni ya uchimbaji madini ya makaa yam awe TANCOAL ya Mbinga,Kampuni ya uchimbaji madini ya urani ya MANTRA ya Namtumbo na kiwanda cha Food Security Company ambapo jumla ya wafanyakazi 400 wamefaidika katika mpango huo.



Hata hivyo anayataja malengo ya chuo hicho kuwa ni  kuanzisha

kozi za zana za kilimo(Agro mechanics) na kozi ya utalii ili kuweza kuunga mkono katika juhudi za serikali za kufungua utalii ukanda wa kusini.

Anazitaja changamoto zinazokikabili chuo hicho kuwa ni ufinyu wa eneo na mgogoro wa ardhi ambayo VETA ilinunua kiwanja kwa ajili ya upanuzi wa chuo ili kuweza kutoa mafunzo kwa walengwa wengi zaidi.

"Changamoto nyingine ni ukosefu wa mabweni kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaotoka nje ya mji wa Songea,Mamlaka inafanya jitihada ili kuwezesha ujenzi wa mabweni kwa ajili ya wanachuo",anasisitiza.

Akizungumza baada ya kukagua chuo cha VETA Songea na kukagua mradi wa chuo cha VETA Namtumbo,Naibu waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia amemwagiza Mtaalamu Elekeziwa Kampuni ya Archquants Service Limited kuhakikisha anawasilisha michoro ya kazi za nje ya Chuo cha ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi Namtumbo ili chuo hicho kiweze kukamilika na kuanza kazi.



Katika hatua nyingine Naibu Waziri Ole Nasha ameitaka Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi VETA kuhakikisha wanaanzisha kozi za utalii na kozi ya ufundi wa zana za kilimo

(agro mechanics) katika Chuo cha Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Songea VETA ili kuweza kupata vijana wengi watakaoweza kusoma kozi hiyo.

Anasema ukanda wa Nyanda za Juu Kusini unategemea sana kilimo na ambapo asilimia 60 ya chakula hutoka huko katika ukanda huo hivyo kuanzisha kozi hiyo itasaidia wananchi wengi kuweza kupata uelewa wa kile wanachokisoma katika kukifanyia kazi.

Anasema Nchi yetu iko kwenye jitihada za kufikia uchumi kati ambao unategemea msukumo wa viwanda na kama unazungumzia masuala ya uchumi wa viwanda ni lazima kuwa na mafundi hivyo Vyuo vya VETA vitasaidia kupata nguvu kazi watakaosaidia katika uchumi wa viwanda.

“Serikali inatilia mkazo Elimu ya ufundi na imejielekeza katika kuhakikisha inapanua fursa ya vijana wengi kupata elimu hiyo na ndio maana unaona Serikali ya awamu ya tano imeamua kuweka Vyuo vya VETA katika kila Wilaya na Mkoa” Alisisitiza Naibu Waziri Ole Nasha

Ameipongeza VETA Songea kwa namna ambavyo wamebuni mbinu mbalimbali za kufikisha Elimu ya ufundi kwa wananchi wengi kwa kuwafikia katika maeneo yao na kuwataka kuendelea kushirikana na kampuni mbalimbali wanapotoa mafunzo yao ili kujua uhitaji wa soko.

**Mwandishi ni mchangiaji wa gazeti hili Mawasiliano yake ni albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917**